

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF AGRICULTURE



TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES
AUTHORITY (TPHPA)



18th December, 2023

TAARIFA KWA UMMA

SITISHO LA MUDA LA UAGIZAJI WA MBEGU ZA MAHINDI KUTOKA MALAWI

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) ni Shirika la Kitaifa la Hifadhi ya Mimea lililo anzishwa chini ya Wizara ya Kilimo kupitia Sheria No.4 ya 2020 ya Afya ya Mimea. TPHPA ina wajibu wa kudhibiti matumizi ya viuatilifu, kutekeleza matakwa ya afya ya mimea, kudhibiti uingizaji na usafirishaji nje mimea na mazao ya kilimo na kuzuia uingiaji na usambaaji wa visumbufu vigeni.

Kupitia upembuzi wa visumbufu hatarishi vinavyoweza kuingia kupitia biashara za mazao ikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo zilizofanyiwa uhandisi geni Tanzania imeweka zuio la muda la kuagiza mbegu za mahindi kutoka Malawi pamoja na zile zinasafirishwa kwenda nchi nyingine kupitia mipaka ya yetu mpaka pale zoezi la upembuzi litakapo kamilika na kiwango cha uhtarishi kimejulikana pamoja na hatua za udhibiti wake.

Kwa sasa Tanzania inazo kanuni zinazo ruhusu majoribio ya mbegu zilizo fanyiwa uhandi geni katika maeneo yaliyowekewa chini ya uangalizi maalumu ambapo hairuhusiwi kuzalisha kwa ajili ya biashara au kwa matumizi ya chakula. Mbegu zote zinazo ingizwa nchini zinapswa kuwa ni mbegu zisizo fanyiwa uhandi geni.

Zuio hili linahusisha usitishaji wa mara moja maombi na utojai wa vibali vyta kuingiza bidhaa husika mpaka pale itakapo amuliwa vinginevyo.

Natanguliza shukurani zetu kwa ushirikiano wenu

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Joseph C. Ndunguru".

Prof. Joseph C. Ndunguru
MKURUGENZI MKUU